Sensa ya viwanda kufanyika Bara na Zanzibar ..Uk.3

tanzaniabora | @tanzaniabora | @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.20 Tanzania Bora JUMATATU Februari 10, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100




# Dkt. Biteko ashauri Uhifadhi wa Qur'an

>> Awataka Waislam kutovunjika moyo wala kukatishwa tamaa

>> Anukuu Aya tofauti akitoa mifano ya Manabii walivyotumia vitabu vitakatifu

>> Ni inayochimbwa nchini yenye thamani ya zaidi ya sh bilioni 570

HABARI UK.2






## Dkt. Samia akerwa na machafuko DRC

NA MWANDISHI WETU

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka DART umesema kuanzia mwezi Machi mwaka huu wa 2025 utasitisha rasmi matumizi ya tiketi za karatasi katika usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka na badala yake watumiaji wote wa Mabasi watatakiwa kutumia kadi janja ambazo zinaendelea kuuzwa katika vituo vikuu vya mradi huo.

Akizungumza Jijini Dar es Salaam wakati wa kuhitimisha mradi wa Maendelezo Yatokanayo

Inaendelea Uk. 2



# Wasira asisitiza CCM itatatua changamoto

HABARI UK.2

# DKT BITEKO ASHAURI UHIFADHI WA QU'AN

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewaasa Waislamu nchini kuendelea kumcha Mungu na kutenga muda wa kujifunza na kuisoma Quríaan Tukufu ambayo itawafunza mambo mema yaliyoelekezwa na Mwenyezi Mungu.

Dkt. Biteko amesema hayo leo Februari 9, 2025 jijini Dar es salaam wakati akizindua Mashindano Makubwa zaidi ya Quríaan Tukufu Ulimwenguni 2025.

ì Nawaomba msivunjike moyo akitokea mwenye tafsiri tofauti nyie msivunjike moyo wala kukatishwa tamaa bali mfanye mashindano haya yawe kinara na kuutangaza uislamu katika ulimwengu,î amesema Dkt. Biteko.

Pia amewahimiza kumuomba Mungu ili Quríaan iwanyanyue na isiwabwage katika shughuli mbalimbali wanazofanya kama kaulimbiu ya mwaka huu inavyosema ì Quríaan Ikunyanyue, Isikubwageî.

Amesema Qur'aan inatoa funzo kwa watu na kuwa waasisi wake waliyaanzisha kwa ngazi ya madrasa lakini baadaye kutokana na umuhimu wake yakavutia wengi zaidi na kuwa mashindano ngazi ya mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi kuwa ya Afrika Mashariki, Bara la Afrika na kisha kufikia ngazi ya kuwa mashindano ya Ulimwengu

ì Mashindano haya mbali na kuwa yanachochea usomaji wa Quríaan Tukufu na hivyo kujenga uelewa wa hofu ya Mwenyezi Mungu lakini pia yanaitangaza Tanzania katika taswira chanya,î amebainisha Dkt. Biteko.

Ameendelea kusema kuwa Nabii Musa aliwalingania watu wake kwa kutumia muongozo kutoka katika Taurati, Nabii Daudi yeye akatumia Zaburi, Nabii Issa (Yesu) akatumia Injili na Mtume Muhamad swalla llahu alayhi wasallam akatumia Quríaan tukufu kuwalingania watu wa umma wake.

"Kimsingi vitabu hivi vya muongozo vinamfundisha binadamu tabia njema na kumsihi kuzishikilia na kumuonesha tabia zisizofaa na kumuasa kukaa mbali nazo.î

Dkt. Biteko amerejea aya katika Quríaan tukufu sura ya 35, Surat Faatir, aya ya 28 ìÖ kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoniî.

Amefafanua ì Aya hii ina maanisha kuwa wale waliopata ujuzi na mafundisho ya Mwenyezi Mungu ambayo yanapatikana katika Quríaan tukufu na kuyazingatia yale waliyojifunza ndio wanaofika daraja la uchamungu.î

Vilevile, Dkt. Biteko ameipongeza Taasisi ya Al-Hikma kwa jitihada zake za kukuza Mashindano ya kuhifadhi Quríaan Tukufu ulimwenguni.

Mkurugenzi Mkuu wa Al- Hikma na Mwenyekiti wa Mashindano ya Quríaan Tukufu Ulimwenguni, Sheikh Nurdin Kishk amesema kuwa mashindano hayo yameendelea kukua kila mwaka kutokana na mapenzi ya kuhifadhi Quríaan.

Aidha, ameishukuru Serikali kwa ushirikiano wake na kwa kuridhia mashindano hayo kufanyika katika Uwanja wa Taifa mnamo Machi 16, 2025 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

ì Mashindano haya yanayofanywa na Al- Hikma Foundation yameweka alama ambayo haitafutika na mataifa mbalimbali yameanza kuyaiga. Pia, Mashindano Makubwa Zaidi ya Quríaan Tukufu Afrika sasa yatajulikana kama Mashindano Makubwa Zaidi ya Quríaan Tukufu kwa Mabara yote ya Ulimwengu ,î amesema Sheikh Kishk

Akizungumza kwa niaba ya Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ali Ngerukwa amesema kuwa Mufti Mkuu yupo tayari kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo ya Ali- Hikma katika kutekeleza shughuli zao.




# WASIRA ASISITIZA CCM ITATATUA CHANGAMOTO

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Mzee Steven Wassira; amewaondoa hofu Wanachama wa chama hicho na wananchi kwa ujumla kuwa changamoto wanakutana nazo zinafahamika na Serikali inayoongozwa na CCM na kwamba hao pia ndiyo wenye jukumu la kuzitafutia ufumbuzi.

Mzee Wassira aliyasema hayo hivi karibuni katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM wilaya Rplya mkoa Mara ambapo aselima mfano wa changamoto za wiyala hiyo ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha Lami, changamoto ambayo tayari ipo katika mipango ya kutatuliwa.

Alisema kuwa CCM kazi yake pamoja na mambo mengine ni kusikiliza kero za wananchi na kuzifanyia kazi kwa vile kufanya hivyo ndiko kutakakoendelea kudumisha mahusiano mema ya wananchi na chama chao tawala.

Amewata wana CCM na wapenzi wa chama hicho kuendelea kuwa na mshikamano ili kuenzi juhudi za Rais wa Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mstari wa mbele kupigania maslahi ya wananchi.

# DKT SAMIA AKERWA NA MACHAFUKO DRC

NA MWANDISHI WETU

HATIMAYE Tanzania meendelea kuwa nchi inayoheshimika katika ukanda wa SADC, baada ya wiki hii kufanyika mkutano wa pamoja wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kujadili na hatimaye kuchukua hatua kufutia mapigano yaliyoshika kasi katika eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wakuu hao kwa kauli moja waliridhia mkutano huo kufanyika nchini Tanzania, chini ya Uenyeji wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, hatimaye umekalimika na kuondoka na maazimio 13 ikiwamo kusitishwa kwa mapigano mara moja katika eneo la Goma, Mashariki mwa nchi ya DRC.

Mkutano huo unakuja siku chache baada ya Tanzania kupokea ugeni mzito uliohusisha takriban Wakuu wa nchi takriban 23 pamoja na Mawaziri 60 na wadau wengine wa Maendeleo kwa ajili ya kujadili matumizi ya Nishati Bora Afrika.

Kwa pamoja heshima hizi zinatokana na juhudi za Rais wa Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan kuifungua nchini kimataifa na kuwa na ushirikiano mwema na nchi mbalimbali duniani.

Katika mkutano huo uliofanyika juzi Jumamosi Februari 8 na kuongozwa na kwa pamoja na Mwenyekiti wa EAC na Rais wa Kenya, Wiliam Ruto na Mwenyekiti wa SADC na Rais wa Zimbabwe, Dk. Emmerson Mnangagwa, uliendelea kuimwagia sifa Tanzania kwa utulivu na amani huku juhudi za viongozi wake wakiweka kipaumbele kuimarisha uchumi.

Mkutano huo, uliohudhuriwa na Marais kutoka jumuiya hizo, ambapo masuala mengine waliyokubaliana ni pamoja na kurejesha huduma muhimu ikiwemo kufungua njia za usambazaji wa chakula na bidhaa nyingine, ili kuhakikisha misaada ya kibinadamu inawafikia walengwa bila kukwama.

Masuala mengine yaliyojadiliwa kwa kina ni utatuzi wa mzozo wa DRC pia kurejeshwa kwa amani kupitia mchakato wa Luanda na Nairobi, huku mkutano huo wa pamoja ukizingatia ripoti ya mkutano wa Mawaziri wa EAC na SADC, kuhusu hali ya usalama Mashariki mwa DRC na kusisitiza ushirikiano ya kisiasa na kidiplomasia ndiyo suluhisho endelevu zaidi la kutatua mzozo eneo hilo.

Mkutano huo wa pamoja umeagiza Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi ya katika nchi za EAC na SADC, kukutana ndani ya siku tano na kutoa maelekezo ya kusitisha mapigano mara moja na bila masharti na kuondoa uhasama.

# Sensa ya viwanda kufanyika Bara na Zanzibar

NA MWANDISHI WETU

SERIKALI ya Tanzania imetangaza kufanya sensa ya uzalishaji viwandani kuanzia Machi hadi Juni 2025, ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika tukio kama hilo kwa wakati mmoja Tanzania Bara na Zanzibar.

Sensa hiyo ambayo mara ya mwisho ilifanyika miaka 12 iliyopita, inalenga kukusanya takwimu katika maeneo manne muhimu ikiwemo usambazaji wa maji safi, mifumo ya kukusanya taka, usimamizi wa taka na shughuli za matumizi ya marudio.

Sekta nyingine zitakazoshughulikiwa ni pamoja na Viwanda, Madini na Uchimbaji Mawe, Uzalishaji wa Umeme na Gesi, na huduma za udhibiti wa hali ya joto.

Waziri wa Viwanda na Biashara wa Tanzania Bw. Selemani Jafo amesema sensa hiyo itakusanya takwimu katika makundi makuu mawili, vinavyoajiri wafanyakazi 10, au zaidi na vile vyenye mfanyakazi mmoja hadi tisa.

# Trump atimua Raia 400 wa India

NA MWANDISHI WETU

MAAFISA wa India wameripoti kuwa raia 104 wa nchi hiyo wamefukuzwa kutoka Marekani kwa kutumia ndege ya kijeshi ambapo hatua hiyo inakuja wakati masuala ya uhamiaji kati ya nchi hizo mbili yameendelea kuibua mijadala, huku wengi wa waliofukuzwa wakidaiwa kuingia nchini humo bila vibali halali.

Aidha ripoti zinaeleza kuwa baadhi ya waliorejeshwa walifungwa pingu wakati wa safari yao, hali iliyozua malalamiko kutoka kwa familia na viongozi wa kisiasa nchini India. Wabunge wa upinzani wametaka serikali kutoa maelezo kuhusu madai ya unyanyasaji dhidi ya raia hao wakati wa kurejeshwa kwao

Waziri wa Mambo ya Nje wa India, Subrahmanyam Jaishankar, amesema kuwa serikali inaendelea kushirikiana na Marekani ili kuhakikisha kuwa raia wa India wanaorejeshwa wanaheshimiwa haki zao. Ameeleza kuwa matumizi ya pingu kwa wahamiaji wanaorejeshwa yamekuwa sehemu ya utaratibu wa Marekani tangu mwaka 2012

Tukio hili limeongeza msukumo wa majadiliano kuhusu uhamiaji kati ya India na Marekani, hasa wakati viongozi wa mataifa hayo mawili wanapojiandaa kujadili masuala ya usalama na sera za uhamiaji katika mazungumzo yanayotarajiwa hivi karibuni




# MKANDARASI DODOMA APEWA ANGALIZO

NA MWANDISHI WETU, DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia miundombinu, Mhandisi Rogatus Mativila amemuagiza Mkandarasi M/s China Geo-Engineering Corporation kuhakikisha anakamilisha ujenzi wa barabara kiwango cha lami Km 10.21, mtaro wa maji ya mvua Ilazo Km 2.1, uboreshaji wa mabwawa ya kuhifadhi maji ya mvua (3), mitaro ya kutiririsha maji Km 2.81 pamoja na ujenzi wa jengo la usimamizi na uratibu wa miradi kwa wakati na ubora.

Mhandisi Mativila ametoa agizo hilo alipokuwa katika ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo jijini Dodoma ambayo inatekelezwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miji Tanzania (TACTIC) chini ya mkopo nafuu toka Benki ya Dunia.

Naibu Katibu Mkuu ameeleza kuwa baada ya ukaguzi wa mradi huo amebaini kuwa ujenzi wa barabara, mifereji ya maji ya mvua pamoja na jengo la usimamizi na uratibu wa miradi upo nyuma ya muda kutokana na nguvu kazi hafifu, ukosefu wa vitendea kazi na kupelekea mradi huo ambao unapaswa kukamilika Februari 2025 kuonyesha ishara za kutofikia malengo ya kukamilika kwa muda na kuwanyima wananchi fursa ya kupata huduma ya barabara.

ìMradi upo asilimia 45% tu bado zimebaki 55% kazi kukamilika, mpaka leo zimebaki siku 13 tu ili mkataba ukamilike. Tumeongea na mkandarasi lakini tumeona sehemu kubwa ya ucheleweshaji wa kazi umesababishwa na mkandarasi mwenyewe kwa kushindwa kuweka nguvu kazi na vifaa vya kutosha, ametueleza anahitaji mwaka mwingine ili akamilishe kazi kikweli ataongezewa muda lakini atapata adhabu ya kukatwa fedha kulingana na mkataba na pia atatakiwa afanye kazi usiku na mchana ili akamilishe kazi ndani ya muda mfupi na kwa ubora ule uleî. amesema.

# Wasira: Msiwatumie vijana wa mara kufanya vurugu



NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Stephen Wasira amesema ni marufuku kwa vyama upinzani kuwatumia vijana kutoka mkoani Mara kama nguvu kazi ya kufanya vurugu katika maeneo mbalimbali.

Amesema CCM inamipango mizuri kuhakikisha vijana hao wanatumia nguvu zao kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kujikwamua dhidi ya umasikini.

Wasira aliyasema hayo jana, alipokuwa akizindua ofisi ya CCM Kata ya Nyakonga wilayani Tarime, Mkoa wa Mara.

ëNataka niwaambie wananchi wa Tarime CHADEMA wakitaka kufanya fujo mahali popote wanakuja kuchukua vijana TarimeÖwanapelekwa kufanya fujo kama majeshi ya kukodi, wakitaka kufanya fujo Mbeya wanakuja, Tarima, wakitaka kufanya fujo sehemu Tarime.

ìTunawaambia vijana wa Tarime wana mvua wana jua na Tarima panalimika, kila kitu kinaota tuwasaidie vijana wa Tarime watumie fursa zilizopoÖtunawaambia CHADEMA muache kuja kuchukua vijana Tarime, sisi sio eneo la mapambano, vijana wetu sio wa kukodisha kwenda katika mapambano, nasema kama mzee wa Tarime waache kuja kuchukua vijana wa Tarime.

Wasira aliwataka vijana wasikubali kuchukuliwa na kutumika katika vurugu kwa kuwa wakienda huko hupigwa, kuumizwa na hata kupata ulemavu kisha kurudishwa Tarime wakiwa na hali mbaya.

ìNasema kama mzee wa Tarime, Mzee wa kimila, muache mambo haya mimi najua yanafanyika siku nyingi,î alisema.

Kwa mujibu wa Wasira, Tarime ukilinganisha na wilaya nyingine za Mkoa wa Mara ina fursa nyingi zaidi, ìhapa tuna madini hapa tuna wachimbaji wadogo na tunataka wachimbaji wadogo walindwe wachimbe kwa amani, tunataka wapewe mafunzo ili wachimbe wapate manufaa kutokana na rasilimali iliyowekwa na mungu katika eneo hili.î

Makamu Mwenyekiti Wasira alisema CCM na serikali yake inataka vijana wa Tarime walime kwa kuwa wanayo ardhi wananchi wengi wa wilaya hiyo wa na ujuzi wa kufuga hivyo wanaweza kuifanya Tarime yote kuwa ya ngíombe wa maziwa.

ìKila familia ikawa na ngíombe wawili wawili ikatufanya tukaweza kujenga kiwanda cha maziwa na watu wa Tarime wakawa wanapata pesa moja kwa moja kila mwezi, hayo ndiyo mambo tunayoyafanya kama Chama,î alisema.

AMTAKA WAZIRI WA MALIASILI AFIKE SERENGETI

Katika hatua nyingine, Wasira amemtaka Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana kufika wilayani Serengeti kushughulikia suala la mahusiano ya wananchi na Hifadhi ya Serengeti.

Alieleza hayo baada ya kupokea kero ya wananchi kuhusu wanyamapori hususan tembo kuvamia makazi na shughuli zao za kilimo.

Alisema ni muhimu waziri husika afike Serengeti, ashughulikie tatizo hilo na kutoa ripoti kwa chama kuhusu hatua zilizochukuliwa.

ìMahusiano ya watu na Tanapa au Gulmet au Ikorongo, hilo nataka kumuagiza waziri wa Maliasili na Utalii aje ashughulikie mahusiano ya watu hao.

ìKwanza suala la wanyama wanaokula mimea ni Tanzania nzima, hilo sio la Mugumu pekee na li akuwa chanzo cha umasikini kwa Watanzania.

ìKwa hiyo tunamtaka waziri mwenye dhamana ashughulikie jambo hilo muda mfupi kadiri inavyowezekana na atuarifu ni nini ambacho kinafanywa,î alisema.

Wasira anaendelea na ziara yake katika mkoa ya Kanda Ziwa leo akitarajiwa kuingia mkoani Simiyu.






# RUVUMA WAAHIDI KUMPONGEZA TENA DKT SAMIA

NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Songea Mjini na Vijijini mkoani Ruvuma, kinatarajia kufanya maandamano yakifuatiwa na mkutano, lengo likiwa ni kuunga mkono maazimio ya Mkutano Mkuu CCM, uliofanyika Dodoma.

Mkutano huo, ulimthibitisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwa mgombea pekee wa urais kwenye Uchaguzi Mkuu, unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Kadhalika, mkutano huo, ulimpitisha Dk. Emmanuel Nchimbi, kuwa mgombea mwenza ambaye wa rais. nchini kwa sasa ni Katibu Mkuu wa CCM Taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Katibu wa CCM wa Wilaya ya Songea Mjini, James Mgego, alisema kuwa CCM Wilaya hiyo, kinaunga mkono mkutano huo utakaofanyika Februari 8, mwaka huu.

Alisema mkutano huo unatarajiwa kufanyiaka viwanja vya Matarawe, Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na wananchi pamoja na wanachama wengine wa CCM.

Alisema kuwa mgeni rasmi wa mkutano huo, anatarajiwa kuwa ni mmoja wa viongozi wa ngazi za juu wa CCM. Hata hivyo hakubainisha jina.

ìNawaomba wananchi kuona umuhimu wa kuhudhuria mkutano huu, kama ilivyo ada kwa ujio wa viongozi wa ngazi ya kitaifa na kufurika uwanjani.

ìMaandamano yataanza majira ya asubuhi yakianzia London, Kata ya Lizaboni, Msamala pamoja na kwenye ofisi za chama Mkoa na yataongozwa na jumuiya zote za chama vijana, Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), pamoja na Jumuiya ya Wazazi.

Dkt Samia amekuwa akifanya mambo mengi yanayohusiana na masuala ya maendeleo na pia uhusiano wa kimataifa mambo ambayo yamekuwa yakiwagusa wananchi moja kwa moja huku wengi wao wakishindwa kuzuia hisia zao na kutamani kumpongeza.

Hivi majuzi Rais Dkt Samia alikuwa Mwenyeji katika kikao cha Wakuu wa nchi za SADC na EAC ambapopamoja na mambo mengine aliwahakikishia Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuwa Tanzania itaendelea kutoa ushirikiano katika kushughulikia mgogoro unaoendelea Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC).

Aidha, Rais Samia ametoa rai kwa Jumuiya hizo mbili kuchukua hatua kuhakikisha kuwa DRC, ambayo ni mwanachama wa EAC na SADC, inakuwa salama na mgogoro unaoendelea nchini humo unamalizika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu Rais Dk Samia ameyasema hayo leo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa EAC na SADC uliofanyika katika Ikulu ya Dar es Salaam ili kujadili hali ya usalama Mashariki mwa DRC.

Rais Samia ameeleza kuwa hali inayoshuhudiwa Mashariki mwa DRC haikubaliki na ipo haja ya kuchukua hatua za haraka kumaliza mgogoro huo unaoleta mateso kwa wananchi.

Aamesema ana imani kuwa Mkutano huo utatoka na maazimio ambayo yatawezesha wananchi wa Mashariki mwa DRC kuishi amani.

Miungoni mwa mambo yanayoonyesha kipaji cha uongizi wa Dkt Samia ni pamoja na uwajibikaji na jinsi anavyokubalika kitaifa kadri siku zinavyokwenda.

## M23 YAPINGA UINGILIAJI WA SADC KIJESHI DRC, YADAI SULUHISHO LIKO NDANI YA NCHI

NA MWANDISHI WETU

KATIKA barua ya wazi kwa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), muungano wa makundi ya waasi na kisiasa nchini Congo la Alliance Fleuve Congo (AFC) unaojumuisha kundi la M23, umejitokeza kupinga vikali uamuzi wa SADC wa kupeleka vikosi vyake Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Katika barua hiyo iliyoandikwa saa chache kabla ya mkutano wa pamoja wa SADC na EAC, AFC inasisitiza kuwa mgogoro wa DRC ni wa kisiasa, wa utambulisho na wa ndani, hivyo unahitaji suluhisho la ndani badala ya maingilio ya kijeshi kutoka nje.

Mratibu wa AFC, Corneille Nangaa Yobeluo, ameandika: ìTunachukua hatima ya nchi yetu mikononi mwetu kwa mujibu wa Katiba ya DRC. Hatuwezi kuruhusu vikosi vya nje kusaidia serikali isiyo halali ambayo inakandamiza watu wake na kuhatarisha umoja wa taifa.î

Katika barua hiyo, AFC inabainisha kuwa M23 ni sehemu ya harakati yao, wakisisitiza kuwa mapambano yao si uasi bali ni mapinduzi ya kikatiba dhidi ya kile wanachokiita ìutawala wa mabavu wa FÈlix Tshisekedi.î Wanaeleza kuwa utawala huo umegeuka kuwa tishio kwa wananchi kwa kujihusisha na ukandamizaji wa kisiasa, rushwa, na kuendeleza siasa za kikabila.

AFC inashutumu vikali SADC kwa kutumia mkataba wa ulinzi wa pamoja (SADC Mutual Defence Pact, 2003) kama sababu ya kuingilia mgogoro huo. Wanasema kuwa mkataba huo unasisitiza kutohusisha majeshi ya nje katika masuala ya ndani ya nchi mwanachama isipokuwa tu pale ambapo kuna uvamizi wa nje.

ìJeshi la SADC linajihusisha na vita vya ndani vya DRC kwa kuunga mkono utawala unaowakandamiza wananchi wake. Huu si ulinzi wa amani, bali ni kuchochea vita vya ndani.î Anaonya Nangaa.

Aidha, barua hiyo inamshutumu Rais wa DRC Felix Tshisekedi kwa kugeuza jeshi lake kuwa chombo cha ukandamizaji wa wapinzani wa kisiasa na kwa kushirikiana na vikundi vya wapiganaji wa kigeni kama FDLR, jambo ambalo AFC inadai kuwa ni tishio kwa wananchi wa DRC na ukanda mzima wa Maziwa Makuu.

# Tanzania mfano wa kuigwa utawala bora



NA MWANDISHI WETU

TANZANIA inazidi kupiga hatua ya kimaendeleo, uchumi unakuwa kwa kasi na maridhiano ya kisiasa ndani ya nchi yanaridhisha, si vibaya kukiri kwamba Rais wa Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan anaenenda vizuri na dhima aliyopewa na Watanzania, kuliongoza taifa sambamba na mahitaji ya Watanzania katika zama hizi.

Anastahili kuwa Rais aliyefanikiwa katika kizazi hiki, maana ukiangalia maboresho na hatua aliyopiga kuyakimbilia maendeleo unaweza kukiri kwamba amepanda zaidi katika mzani kwani hakuna awamu unayoweza kuinasibisha, bali inabaki kuwa na msemo wa kila zama na historia yake.

Mara nyingi ninapoandika makala hizi nikielezea hali ilivyokuwa enzi za utawala wa Awamu ya Kwanza chini ya Uongozi wa hayati Mwalimu Julisu Nyerere, hoja zinmazofuata zinaelekezwa katika masuala ya maendeleo yalichelewa hivyo si wakati sahihi wa kufananisha awamu hizi.

Kwangu si hoja ya msingi, maana yanakwenda kwenye masuala ya utekelezaji, mafanikio au kushindwa, maeneo ambayo yapo nje ya hoja zangu.

> *Ni wale wanaopata vyeo na kutohisi kuwa Tanzania ni ya kila mwananchi na rasilimali hizi zipo kwa ajili ya kizazi hiki, kulingana na mahitaji ya kihistoria ya uzawa!*

Kiu ya Makala hii ni kuweka ‘Jicho Kongwe’ katima vichwa Chipukizi vya vijana wa leo, ambao ndiyo asilimia kubwa ya Watanzania kwasasa, wapate ufahamu juu ya kule tulikotoka na huku twendako!

Lakini huwa siweki shaka hata robo kuwa nitakuwa Majununi kama nitathubutu kuyafananisha maendeleo, mfano yale ya awamu ya kwanza na hii ya sita maana kila kitu kimepishana kwa hatua kubwa.

Siyo mantiki yangu kuorodhesha yale yaliyofanikiwa katika utawala wowote wa nchi hii, iwe Awamu ya Kwanza hadi ya Sita, Miongoni mwa Watakwimu mimi simo.

Japokuwa ukiniuliza mafanikio yasiyohitaji tathmini au kuingia kwenye ‘Vijaruba’ vya watunza kumbukumbu nitakujibu kuwa ni “Mama anaupiga mwingi’ na ukitaka mifano nitakutembeza na kukuonyesha vidhibiti mfano Reli ya Kisasa, Nitakupeleka ukaone maendeleo kule Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere na maeneo mengine ambayo huko awali nisingepata fursa kama hii.

Lakini ukiuliza siri ya urithi wa utulivu wa Taifa nitarudi kwenye vitabu na kukumbusha jinsi Mwamu Nyerere alivyofanya makubwa kwawakati wake, kufurika kwa viwanja kujenga umoja baina ya wananchi kwa kupinga ukabila na Udini na mambo mengine yaliyostahili katika taifa hili changa.

Huu mseto wa makabila mfano Mzanaki kuzaa na Mpemba, Mmakonde kupata mke katika familia ya Wanyiramba, haikuwa kazi nyepesi, juhudi hizi ndiyo mafanikio tunayoyanadi kuwa ni mafanikio ya Utawala wa Mwalimu Julius Nyerere.

Ukiacha eneo hilo pia tunaangalia jinsi Watanzania walivyoshiriki kwa nguvu zote kupigana vita dhidi ya maadui watatu wa Taifa, Ujinga, Umasikini na Maradhi.

Maadui hawa watatu hata kama waliisumbua jamii ya Watanzania toka nchi ilipopata Uhuru Tarehe 9 Desemba 1961 hadi hhivi sasa, lakini enzi hizo kila Mtanzania mwenye akili timamu, alifahamu jukumu lake la kupambana na maadui hawa.

Hii ilitokana na Somo la Uzalendo jinsi lilivyowaiingia Watanzania na msingi wake ulijengwa katika elimu iliyokuwa ikitolewa, tangu kwa wanafunzi wa masomo ya awali hadi vyuoni, swali la kuwajua Maadui Watatu wa Taifa halikuhitaji mwanafunzi afike darasa fulani, hata anayesoma chekechea aliweza kuwataja bila ya kumeza mate.

Hii ilisaidia jamii ya kujifunza uzalendo na kukataa kuishi katika mambo yanayotajwa kama ni miiko ya Taifa, mfano Kutoa au Kupokea Rushwa, kutumia cheao kwa faida ya mtu binafsi, na mengine yaliyokuwa katika nukuu za Ahadi 10 za Mwana TANU, Watanzania waliyabeba kama mzigo wao.

Leo hii ukiukwaji mkubwa wa haki za Binadamu, ukosefu Maadili, kutochukia Rushwa na Ufisadi ni mazao ya vijana wetu walioamua kuyapa kisogo, masomo ya uzalendo.

Ni wale wanaopata vyeo na kutohisi kuwa Tanzania ni ya kila mwananchi na rasilimali hizi zipo kwa ajili ya kizazi hiki, kulingana na mahitaji ya kihistoria ya uzawa!

Tunaweza kukiri kuwa tumechelewa, lakini bado tuna nafasi ya kufika, kwani miguu yetu ingalipo safarini.

Tuendelee kushukuru kwa kila hatua, mengi ya Awamu wa Sita yanatufumbua macho, kuona yale tuliyohisi kiasili yanapaswa kuonekana Ulaya tu, leo Afrika na hususan Tanzania tunazungumza sauti moja na wale wanaosihi Texas.

Akikwambia kuwa alipanda Treni la Umeme kutoka Texsan kwenda Miami hutoshangaa ilivyokuwa kwani na wewe unamiliki usafiri huo katika nchi yako.

Aliyewahi kuona awamu zote za nchi hii hawezi kumaliza maneno bila kumuombeas dua huyu Mama aliyeshika kijiti Awamu ya Sita kwani maneno kwake yamekuiwa machache zaidi ya vitendo.

Mungu Ibariki Tanzania.

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakukuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


### BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

### MAWASILIANO

JAMVI MEDIA GROUP




*Wapigania uhuru wa Afrika na wanaharakati wa ukombozi wa Kusini mwa Afrika wakiwa katika picha ya pamoja kutoka kushoto Oliver Tambo wa Afrika Kusini, Sam Nujoma wa Namibia, Keneth Kaunda wa Zambia na Julius Nyerere wa Tanzania. Kwa sasa hawa wote ni marehemu ambapo aliyefunga pazia ni Sam Nujoma aliyefariki jana.*

# UCHAMBUZI

## Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI
DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# AFYA YA MAMA NA MTOTO SERIKALI INASTAHILI PONGEZI



NA MWANDISHI WETU

YAPO mambo mengi yanayoendelea kuwa kumbukumbu ya akina Mama na Watanzania yaliyo ya faraja kwao katika uongozi wa Awamu wa Sita, chini ya uongozi wa Dkt Samia Suluhu Hassan, ikiwemo maboresho makubwa katika sekta ya afya hasa matibabu ya akina mama na watoto.

Kwa kiasi kikubwa akina mama katima maeneo mengi mijini na Vijijini walikuwa katika kilio cha kukosa huduma za afya na hasa kukosekana kwa zahanati na vituo vya afya vilivyokuwa na sifa ya kufikika kirahisi na kupata huduma ya kujifungua.

Kilio hiki kilikuwa ni moja ya vipaumnbela vya awali kwa Rais Dkt Samia muda mfupi alipoingia madarakani, kwani alianza kuchukua hatu na ilipotimia miaka mitatu ya uongozi wake, akaogeza bajeti maradufu kwa sekta afya ili Mama na Mtoto wanufaike kwa kupata huduma ya afya, tena zikiwa karibu na maeneo waishio.

Kwa kipindi hicho kifupi cha utawala wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mohamed Mchengerwa, alibainisha kuwa hadi kipindi cha mwezi Septemba mwaka jana, kulikuwepo na jumla ya Hospitali za Wilaya 129 zilizokamilika kujengwa nchini kote, idadi ambayo kwa sasa imeongezeka.

Hii ilikuwa ni miungoni mwa mafanikio makubwa ya uwekezaji wa miundombinu ya afya ikiwemo vituo vya huduma za afya ambavyo vimeongezeka kutoka 8,549 alipokuwa anaingia madarakani mwaka 2021 hadi 9,610 Machi mwaka mwaka jana hili likiwa ni ongezeko la vituo 1,061, id adi kubwa kupata kutokea katika historia ya Tanzania.

Kufuatia maboresho hayo iliwezesha wajawazito waliojifungua kwenye vituo vya huduma za afya kuongezeka kutoka asilimia 63 mwaka 2021 hadi asilimia 85 mwaka mwaka 2023 nayo ni idadi kubwa na ya kupigiwa mfano katika mafanikio yaliyopatikana katika utawala huu wa Awamu ya Sita.

Haya ni malengo ya awali huku mipango ikiwa ni kufikia asilimia 95 ili Mama waweze kujifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya ifikapo mwaka 2030. hii ni ni mipango inayoendelea kupewa msukumo ili iweze kuwakomboa akina Mama wa Tanzania waliokuwa katika mashaka makubwa kutokana na kukosekana kwa huduma bora ya afya kwa Mama na Mtoto.

Lengo kuu kwa sasa ni kupunguzwa kwa vifo vya wajawazito vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104.Pia, inatajwa kuwa mageuzi hayo ya Rais Dkt. Samia, ni kwamba vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, vimepungua kutoka 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi 33 mwaka jana.

ìVifo vya watoto wachanga (wenye umri wa chini ya siku 28) vimepungua kutoka 25 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi vifo 24 kwa vizazi hai 1,000 hadi sasa, ì inaeleza taarifa hiyo ya Wizara ya Afya.

Eneo lingine la ufafanuzi wa wizara, ni kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano vifo vyao vimepungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 na kufika 43 mwaka 2022.

Hapo ndipo inapozaliwa swali la msingi, kuna hatua na mikakati ipi inayofanyika kufikisha mahali hapo?

UMIRAISHAJI HUDUMA

Wizara ya Afya katika taarifa yake in ufafanuzi kwamba, kati ya mwaka 2021 hadi Machi jana, Serikali ya Awamu ya Sita ikaendelea kuwekeza katika huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, katika maendeleo kadhaa;

Hapo kuna rekodi ya kukamilishwa ujenzi wa jengo kongwe la huduma za afya ya mama na mtoto, katika hospitali kongwe ya Meta, jijini Mbeya ikigharimu shilingi bilioni 13.2.

Pia, kuna uendelezaji wa majengo ya Mama na Mtoto, kwenye hospitali za rufani za mikoa ambazo ni; Sekou oure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu jumla ya shilingi bilioni 71.1.

Kuna kuimarishwa huduma za upasuaji wa wajawazito kwa kuongeza, vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kwa mjamzito (CEMoNC) kutoka vituo 340 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 523 mwaka 2023. Ni ziada ya 183.

Kuanzisha wodi maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Units - NCU); hadi kufikia Desemba 2023, kuna jumla ya hospitali 189 zinatoa huduma za NCU ikilinganishwa na hyospitali 165 mwaka 2022 na Hospitali 14 tu mwaka 2018.

Kumekuwapo uimarishaji, upatikanaji wa bidhaa za afya na uzazi, mama na mtoto, katika vituo vinavyomilikiwa na serikali, ukiongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 Za mwaka 2023.

Kuimarishwa huduma za Saratani ya Mlango wa Kizazi; kukiwapo jumla ya mashine 140 za uchunguzi wa saratani zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo 140 vya kutoa huduma za afya katika halmashauri 104, katika mikoa 26. Vifaa vyote vina thamani ya shilingi bilioni 1.1.

Mfumo wa M-mama; Serikali ya Rais Dk. Samia, imeanzisha mfumo wa kieletroniki unaoratibu rufani, kwa kusafirisha wajawazito na watoto wachanga wanaohitaji huduma za dharura.

Hiyo ni safari kutoka ngazi ya jamii hadi vituo vya kutoa huduma za afya au kutoka kituo cha ngazi ya chini, kwenda ngazi ya juu.

Kati ya mwaka 2022 hadi 2023, mfumo huo umeendelea kufanya kazi katika mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar, kukiwapo wahusika 46,941 wamenufaika na huduma za dharura za rufani.

Wizara ya Afya kupitia ripoti yake mwaka jana, inatamka uwekezaji uliofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hasssan, katika kuimarisha ubora wa huduma za afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, viashiria vya nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tanzania ikangíara kufanya vizuri kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto.

*Picha mbalimbali zikimuonyesha Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Kenya, William Ruto akiondoka nchini Tanzania baada ya kuhudhuria mkutano wa SADC na EAC uliofanyika jijini Dar es Salaam, juzi.*










*Picha mbalimbali zikimuonyesha Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Kenya, William Ruto akiondoka nchini Tanzania baada ya kuhudhuria mkutano wa SADC na EAC uliofanyika jijini Dar es S alaam, juzi.*

# CCM ITASHINDA KWA UTEKELEZAJI ILANI



NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi waliibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

> Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# M23 waibuka na hoja mpya dhidi ya SADC, EAC

NA MWANDISHI WETU



KATIKA barua ya wazi kwa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), muungano wa makundi ya waasi na kisiasa nchini Congo la Alliance Fleuve Congo (AFC) unaojumuisha kundi la M23, umejitokeza kupinga vikali uamuzi wa SADC wa kupeleka vikosi vyake Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Katika barua hiyo iliyoandikwa saa chache kabla ya mkutano wa pamoja wa SADC na EAC, AFC inasisitiza kuwa mgogoro wa DRC ni wa kisiasa, wa utambulisho na wa ndani, hivyo unahitaji suluhisho la ndani badala ya maingilio ya kijeshi kutoka nje.

Mratibu wa AFC, Corneille Nangaa Yobeluo, ameandika: ìTunachukua hatima ya nchi yetu mikononi mwetu kwa mujibu wa Katiba ya DRC. Hatuwezi kuruhusu vikosi vya nje kusaidia serikali isiyo halali ambayo inakandamiza watu wake na kuhatarisha umoja wa taifa.î

Katika barua hiyo, AFC inabainisha kuwa M23 ni sehemu ya harakati yao, wakisisitiza kuwa mapambano yao si uasi bali ni mapinduzi ya kikatiba dhidi ya kile wanachokiita ìutawala wa mabavu wa FÈlix Tshisekedi.î Wanaeleza kuwa utawala huo umegeuka kuwa tishio kwa wananchi kwa kujihusisha na ukandamizaji wa kisiasa, rushwa, na kuendeleza siasa za kikabila.

AFC inashutumu vikali SADC kwa kutumia mkataba wa ulinzi wa pamoja (SADC Mutual Defence Pact, 2003) kama sababu ya kuingilia mgogoro huo. Wanasema kuwa mkataba huo unasisitiza kutohusisha majeshi ya nje katika masuala ya ndani ya nchi mwanachama isipokuwa tu pale ambapo kuna uvamizi wa nje.

ìJeshi la SADC linajihusisha na vita vya ndani vya DRC kwa kuunga mkono utawala unaowakandamiza wananchi wake. Huu si ulinzi wa amani, bali ni kuchochea vita vya ndani.î Anaonya Nangaa.

Aidha, barua hiyo inamshutumu Rais wa DRC Felix Tshisekedi kwa kugeuza jeshi lake kuwa chombo cha ukandamizaji wa wapinzani wa kisiasa na kwa kushirikiana na vikundi vya wapiganaji wa kigeni kama FDLR, jambo ambalo AFC inadai kuwa ni tishio kwa wananchi wa DRC na ukanda mzima wa Maziwa Makuu.

ìTshisekedi amebadilisha nchi kuwa uwanja wa vita kwa maslahi yake binafsi. Familia yake inadhibiti maeneo yote ya madini nchini, huku akitumia mgogoro huu kama mbinu ya kulinda biashara yao ya rasilimali za taifa,î inasomeka sehemu ya barua hiyo.

AFC inahimiza wakuu wa SADC na EAC kufikiria upya uamuzi wao wa kupeleka majeshi na badala yake kuhamasisha suluhisho la kisiasa. Wanataka mazungumzo ya moja kwa moja kati ya harakati yao na serikali ya Kinshasa ili kupata mwafaka wa kudumu. ìSuluhisho la mgogoro huu haliko nje ya DRC, lipo ndani ya watu wa Kongo wenyewe,î inasema AFC.

Kwa mujibu wa AFC, ili kurejesha amani nchini, Tshisekedi anatakiwa kuacha kutumia mamluki wa Ulaya kuwaua raia wa Kongo, kuacha kufadhili FDLR, na kusitisha ushawishi wa kijeshi unaolenga kuendeleza siasa za kikabila.

Barua hiyo inahitimisha kwa wito kwa jumuiya za kimataifa, viongozi wa Afrika, na wananchi wa DRC kusimama kidete dhidi ya kile wanachokiita ìudikteta wa Kisasaî wa Tshisekedi na kuhakikisha kuwa mustakabali wa taifa hilo unaamuliwa na wananchi wake wenyewe, si kwa mizinga ya mataifa jirani au makubaliano ya kisiasa yanayopuuza uhalisia wa



# DAKTARI MBOBEZI ATOA NJIA YA KUDHIBITI UGONJWA WA KISUKARI

NA MWANDISHI WETU



DAKTARI ni profesa, Daktari wa sayansi mtaalam katika idara ya Endoknolojia .

Dk. Zoli N'Damdi anakiri kujua njia ya siri ya kudhibiti ugonjwa wa kisukari ambayo huzuia madhara ya kisukari katika hatua yoyote.

Ripota wetu alimhoji daktari maarufu Dkt. Zoli N'Damdi. Daktari alielezea kwa undani kuhusu mbinu za kisasa za kujikinga na kisukari.

Mwandishi wa habari: Mara kwa mara umesema kwamba kutoa sumu kwenye kongosho kwa ajili ya kudhibiti na kujikinga dhidi ya ugonjwa wa kisukari kwa ufanisi. Kwa nini unafikiri hivyo?

Dkt. Zoli N'Damdi: Ni rahisi. Utendaji kazi wa viungo na mifumo yote katika mwili wa binadamu hutegemea ubora wa usambazaji wa damu kwenye viungo na mifumo hiyo.Usambazaji wa damu huhakikisha upatikanaji wa oksijeni na virutubisho kwenye seli zote na tishu, pamoja na utoaji wa kaboni dioksidi na bidhaa nyingine za kimetaboliki kwenye viungo vya ndani. Unapokuwa mdogo, unapokuwa katika ujana unakuwa na mishipa mingi ya damu mpya. Katika umri huo unakuwa unatumia lishe bora. Lakini kadri unavyozeeka, ndivyo unavyosonga kidogo, na mishipa ya damu huanza kuwa chafu. Hii ni kwa sababu ya sababu nyingi, sio tu hatari (kama vile kuvuta sigara, lishe duni, ikolojia, maisha ya kukaa), lakini pia asili kabisa (kwa mfano, uwekaji wa cholesterol kwenye kuta za mishipa ya damu, ambayo hufanyika kwa watu wote).



Inamaanisha nini mishipa ya damu inapokuwa imechafuka? Hebu fikiria mabomba ambayo hayajasafishwa kwa muda mrefu. Nini kitatokea ? Matokeo yake bomba litajaa kutu ambazo haziwezi kuyeyeka na maji yanakuwa hayana ladha. Kitu kama hichi kinatokea kwenye viungo vyetu vya ndani. Kolesteroli au vitu vingine vinapojikusanya kwenye mishipa ya damu, damu huchafuliwa na usambazaji wa damu hauwi kama kawaida. Matokeo yake viungo na mifumo yote huathiriwa na kushindwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Kitu kama hichi pia hutokea kwenye kongosho. Kongosho huzalisha insulini ambayo huvunja vunja sukari kwenye damu. Mishipa ya damu inapoziba kongosho haiwezi kufanya kazi

Inaendelea Uk. 13

# DAKTARI MBOBEZI ATOA NJIA YA KUDHIBITI UGONJWA WA KISUKARI

Inatoka Uk. 12

yake hivyo seli pia hushindwa kuitikia ipasavyo kwa insulini.

Kama unasafisha kongosho mara kwa mara unaweza kuishi hadi miaka 80 na usipate ugonjwa wa kisukari.Hautalazimika kuvumilia maumivu na ubongo wako utafanya kazi vizuri. Unaposafisha mishipa ya damu, umri wa kuishi utaongezeka na afya itaimarika sana. Na hii sio nadharia tu.Kutokana na uchunguzi niliofanya , teknolojia mpya na uzoefu wangu katika idara ya wa endoknolojia niliweza kupata suluhisho.

Hivi ndivyo uchafuzi wa mishipa ya damu hutokea hatua kwa hatua. Doa jeupe ni hatua ya ukandamizaji ambayo inazuia seli kuingiliana na insulini. Matokeo yake, kunakuwa na glukose ya ziada mwili.

Mwandishi: Ni nini maoni yako kuhusu kuongezeka kwa viwango vya sukari ?

Dkt. Zoli N'Damdi: Hii huathiri mwili mzima. Lakini inathiri zaidi viungo na mifumo ambayo ina mfumo imara wa mishipa .

Ugonjwa wa kisukari husababisha magonjwa kama vile:

Diabetic retinopathy.

Ugonjwa wa mguu wa kisukari. Mara nyingi husababisha mguu kukatwa.

Kupungua kwa mishipa kwenye sehemu za chini huitwa ugonjwa wa ateri ya pembeni, au PAD. Dalili za msingi kuu ni baridi na kuwashwa ikifuatiwa na matatizo ya polio.

Husababisha thrombosis na magonjwa ya mishipa ya pembeni. Baada ya muda uharibifu wa mishipa ya damu husababisha kalsiamu kwenye mishipa ambayo husababisha atherosclerosis.

Uharibifu wa figo. Uharibifu wa mishipa ya damu husababisha ongezeko la mara kwa mara la sukari kwenye damu, ambayo pia huathiri sana mishipa midogo ya damu (kapilari) iliyo kwenye figo.

Ili kukusaidia kuelewa hatari za ugonjwa wa kisukari, nitakuonyesha baadhi ya picha.

Ugonjwa wa kisukari husababisha huoni hafifu au upofu kabisa

Ugonjwa wa mguu wa kisukari. Katika picha unaweza kuona hatua zote za hali hii ikiishia na



kukatwa kwa kidole.

Damu kuvilia kwenye jeraha na kuziba kwa mishipa ya pembeni ya miguu na mikono.

Ugonjwa huu ni vigumu sana kuepukika. Nchini Tanzania, idadi ya vifo vinavyotokana na matatizo ya kisukari ni mara 4 zaidi nchi nyingine. Wataalam wanajua: ni muhimu kusafisha kongosho kwasababu husidia kuoresha mchakato wa kuvunja vunja glukose. Lakini kwa sababu fulani njia hii bado haipo katika nchi yetu.

Watu hawawajibiki kutumia njia mpya na wagonjwa wanatumia dawa ambazo ni za kutumia maisha yote. Lakini dawa hizi hazisaidii sana kudhibiti mzizi wa ugonjwa huo bali husidia kutuliza kwa muda tu. Ni muhimu kusafisha mishipa ya damu! Hta hivyo huko Ulaya watu wote wenye umri wa miaka 35-40 wamekuwa wakisafisha mishipa ya damu kwa zaidi ya nusu karne. Kwa nini watu wa nchini kwetu hawajui lolote kuhusu njia hii? Hili bado ni swali kubwa kwangu.





# HAPA NDIPO MTEGO WA SIMBA ULIPO

>> Inatoka uk. 16

Bado Chasambi ana nafasi ya kurejea katika ubora na kuwa imara zaidi licha ya kujifunga kwenye mchezo wa ligi mbele ya Fountain Gate wakigawana pointi mojamoja ndani ya dakika 90.

Ipo wazi kwamba kwenye mchezo ule uliochezwa Februari 6 2025 ni yeye alitoa pasi ya bao kwa Ateba ambaye alifikisha jumla ya mabao 8 ndani ya ligi ni yeye alirudisha pasi yenye ujazo mkubwa kwa kipa Moussa Camara ambaye alikwama kuipata pasi hiyo mwisho ikawa bao la usawa.


Imeandikwa na Lunyamadzo Mlyuka, Mtunzi kitabu cha Ganzi ya Maumivu Kwenye Upendo, kukipata TUNAOMBA ODA 0756 028 371. Ni simulizi inayozungumzia maisha ya Kiafrika, usaliti, visa, furaha. Wakazi wa Njombe kitabu kinapatikana Mtaa wa Mpechi kwa Chris Jabari, Kigamboni kwa Tupokigwe, Posta karibu na Mnara wa Askari ukiwa unaelekea chuo cha IFM.

## RASHFORD ATUA ASTONVILA

BARCELONA, HISPANIA

WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford wamekutana na viongozi wa Antonvila siku ya Jumanne huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akitafuta njia ya kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Rashford kumekuwa na uvumi wa kutakiwa na timu kadhaa, hivyo kuzidi kufanya uvumi wa kuondoka kwake kushika kasi zaidi, huku hayo yakija wakati Paul Scholes akisema, ndani ya kikosi hicho kuna wachezaji wanane wabovu.



## LUIZ ANAKWENDA HAPA

MILAN, IITALIA

TIMU ya Juventus wameipa Chelsea fursa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal.

Hayo yaja huku kiungo wa Ufaransa Paul Pogba, 31, anazingatia ofa kadhaa kutoka kwa timu za ligi tano kuu za Ulaya, lakini makubaliano ya mkataba hayajafikiwa.



# P-SQUARE
## 'Mapacha' ndani ya mgogoro!-5

LOGOS, NIGERIA

Ni lazima nieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, "aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. "Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza."

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. "Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha."

# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'

# Tamasha la muziki 'Kadanse ya Mama' yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.

Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.

Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz 'Wanamsondo ngoma' ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.





UK. 15

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA
# MICHEZO

JUMATATU Februari 10, 2025

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz

# Simba yachungulia mechi ya Yanga vs JKT



NA MWANDISHI WETU

YANGA leo itakuwa na kibarua kizito itakapoivaa JKT Tanzania katika Uwanja wa Jenerali Isamuhyo, Mbweni Jijini Dar es Salaam, huku mahasimu wao Simba wakitamani kuona wapinzani wao hao wakipoteza mechi hiyo.

Simba wanaitazama kwa jicho la tamaa mechi hiyo huku wakielekeza dua zao kwa kikosi cha JKT kiweze kuibuka na ushindi ili kuwasimamisha mabingwa hao watetezi, wawe na uwiano mdogo wa tofauti ya pointi.

Yanga hadi sasa inaongoza Ligi ikiwa na pointi 45 ambazo ni pungufu ya pointi moja dhidi ya watani wao Simba yenye Pointi 44

Inaendelea Uk.14

# Yanga yamchongea Chasambi Simba

NA MWANDISHI WETU

KINDA la Msimbazi aneyekuja vizuri katika medani ya Soka la Tanzania Ladack Chasambi, bado yupo katika wakati mgumu akipokea hisia tofauti kutoka kwa mashabiki baada ya kuisababishia timu yake kutoa sare 1-1 dhidi ya Fontain Gate mmchezo uliopigwa Jumatano iliyopita.

Chasambi alifunga bao katika harakati za kumrudhishia kipa dakika za mwicho za mechezo huo wakati timu yake ikiwa mbele kwa bao 1-0.



Kufuatua tukio hilo lililomfedhehesha chipukizi huyo kiasi cha kutoa machozi uwanjani, mashabiki wa timu hiyo wamegawanyika baadhi wakiwa upande wa Chasambi kuwa alifanya tukio hilo kwa makosa, wengine wakimkalia kooni wakidai kuwa lilikuwa ni tukio la kusudi.

# HAPA NDIPO MTEGO WA SIMBA ULIPO

NA MWANDISHI WETU

ENEO la ushambuliaji litawaangusha Simba kwenye mbio za kuwania ubingwa ikiwa wachezaji watashindwa kuwa makini hasa katika umaliziaji wa nafasi na kutengeneza nafasi.

Katika michezo ambayo ameanza Mpanzu ameonekana kuwa na shauku kubwa yakutaka kufunga zaidi ya kutengeneza nafasi za mabao jambo linalowapa ugumu Simba kufunga ndani ya uwanja.

Nafasi ambazo wanazipata ndani ya 18 ni aghalabu kuzitumia zote kwa usahihi, kwa mfano mchezo dhidi ya Fountain Gate, Leonel Ateba alipata nafasi zaidi ya tano akatumia nafasi moja. Mchezo dhidi ya KenGold, Joshua Mutale ndani ya 18 anashindwa kupiga shuti kulenga lango.

Mpanzu alikuwa na nafasi kutoa pasi zaidi ya pasi tatu zote akaamua kufunga mapigo yakawa ni hasara kwa timu.

Jean Ahoua akiwa ndani ya 18 anapiga shuti ambalo hata yeye mwenyewe anashangaa amepigaje nibkazi kubwa inahitajika eneo la kiungo na eneo la ushambuliaji kufanyiwa kazi bila kusahau back pass.

Chasambi hakuwa na siku nzuri tangu dakika za mwanzo ndio maana mapigo yake matatu ya kona yote yalikuwa hovyo.

Inaendelea Uk.14



GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM